OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE,

SEKONDARI YA TOANGOMA

S.L.P 100221, DAR ES SALAAM.

Tarehe ……

Kumb. Na MEVT/S.2215/U

YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI</u>

1.0 UTANGULIZI

Napenda kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari Toangoma HONGERA SANA.

1.1 KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe …… fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Baada ya wiki mbili toka tarehe ya shule kufunguliwa nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine

1.2 MAHALI ILIPO

Shule ya Sekondari Toangoma ipo kata ya Toangoma eneo la viwanja vipya vya Serikali katika manispaa ya Temeke. Panda magari ya Temeke Toangoma au Kigamboni Toangoma. Shule ipo mita 500 kutoka stendi ya Toangoma. Fuata vibao.

2.0 USAJILI

Unatakiwa ufike shuleni tarehe…….. asubuhi saa mbili upate kusajiliwa na kupatiwa maelezo kuhusu shule ukiwa pamoja na mzazi wako.

3.0 SARE YA SHULE

3.1 WASICHANA

- Sketi mbili za kijivu. Zishonwe kwa mtindo wa rinda boksi (angalia mfano) ziwe ndefu zinazofunika magoti. zisiwe na belt (mkanda) mpana
- Shati mbili nyeupe tetroni mikono mifupi
- Viatu vya ngozi jozi mbili, vyeusi visiwe na visigino virefu wala visiwe wazi juu. Pia visiwe na urembo wowote.
- Tai mbili za kijivu
- Soksi nyeupe, jozi mbili ndefu zinazokaribia magotini.
- Hijabu:- uvaaji wa Hijabu ni hiyari. Zishonwe kwa maelezo ya fuatayo
  - i) Hijabu (ushungi) iwe ya tetron nyeupe isiyo na maua ishonwe kwa ntindo wa solo, ifunike mabega, isivaliwe kwa mtindo wa ushungi na isiwe na less pembeni.
  - ii) Punjabu dress (blauzi) nyeupe iwe pana, shingo ya duara mikono mirefu na iwe ndefu inayofika magotini.

iii) Sketi rangi ya kijivu mshono wa rinda boksi iwe ndefu inayofika miguuni (iguse kifundo cha mguu)
iv) Kitambaa cha mfano (grey no 1) kimeambatanishwa.
v) Sweta la kijivu (kama atahitaji)

3.2 WAVULANA

- Mkanda mweusi wenye kifungio cha kawaida (kisicho na urembo)
- Suruali mbili za kijivu zishonwe kwa kuzingatia maelezo. Mtindo wa jeans hauruhusiwi kabisa na zisiwe modals
- Mashati mawili meupe ya tetroni mikono mifupi
- Viatu jozi mbili vyeusi vya ngozi vinayofungwa na kamba visivyo na urembo wala kisigino kirefu. Viatu vya wazi haviruhusiwi
- Tai mbili za kijivu
- T-shirt kijivu na kaptula (angalia mfano) kwa ajili ya michezo
- Soksi nyeusi ndefu, jozi mbili
- Nembo mbili za shule
- Kitambaa cha mfano (grey no 1) kimeambatanishwa.
- Sweta la kijivu (kama atahitaji)

3.3 UVAAJI WA SARE

Sare ya shule ivaliwe katika mazingira yafuatayo

- Wakati wa masomo.
- Mwanfunzi atokapo nje ya shule
- Katika mikutano yote ya shule na mikutano ya hadhara
- Siku zisizo za shule (jumamosi) anapokuja shuleni

3.4 NGUO ZA MICHEZO

Wavulana

- Bukta na fulana rangi nyeusi na Raba

Wasichana

- Track rangi nyeusi na fulana ya kijivu
- Raba nyeupe

3.5 UNADHIFU

- Muda wote sare safi na iliyonyooshwa
- Wavulana na wasichana wote wakate nywele ziwe fupi. Hairuhusiwi kusuka

4.0 MENGINEYO MUHIMU

Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi yanakutegemea zaidi wewe mzazi/ mlezi. Ni imani yetu utampatia mwanao kila aina ya msaada ili aweze kusoma kwa makini.

4.1 VIFAA VINGINE BINAFSI

i. Ream 1 A4 (awe nayo kwa ajili ya mazoezi na mitihani)
ii. Bag la kubebea vitabu (chool bag) jeusi
iii. Mkebe 1 (MATHEMATICAL SET)
iv. Peni, Pensel na rula
v. Aje na picha za passport size nne

4.2 Simu ya mkononi hairuhusiwi

5.0 MAKOSA YAFUATAYO USABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

A. Wizi
B. Uasherati na ushoga
C. Ubakaji
D. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
E. Kucheza kamari
F. Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
G. Kudharau Bendera ya Taifa
H. Kuwa mjamzito, kupata mimba msichana/ kusababisha ujauzito
I. Kuoa au kuolewa
J. Kutoa mimba
K. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
L. Kukataa adhabu kwa makusudi
M. Kuwa na simu ya mkononi

6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ua Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi – Tamisemi yenye Jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utazopewa
d. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
f. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
g. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
h. Kutunza mali za umma

7.0 MAHUDHURIO

i) Kila mwanafunzi ni lazima afike shuleni asubuhi 12:30 na kufanya usafi wa mazingira na kuhudhuria gwaride na ukaguzi wa usafi wa kuchemsha mwili
ii) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali/ ruhusa kutoka kwa mwalimu wa darasa au wa zamu
iii) Mwanafunzi haruhusiwi kutokuhudhuria shuleni bila kupata kibali, ruhusa itatolewa kwa sababu maalumu tu kwa ombi la mzazi/ mlezi. Mwanafunzi

akikosa zaidi ya siku tatu mfululizo atalazimika kufika pamoja na mzazi/ mlezi aliye andikishwa.

iv) Mwanafunzi ni lazima afanye mitihani yote aliyosoma.

v) Kila mwanafunzi yampasa kuhudhuria vipindi vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonyweshwa kwenye ratiba.

vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa na kazi za mikono.

vii) Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka na bila kuchelewa.

8.0 VITU VISIVYORUHUSIWA

1. Pete.
2. Kunyoa nyusi.
3. Hereni.
4. Kupaka rangi.
5. Kucha ndefu.
6. Kusuka nywele.
7. Kukali au kulilax.
8. Hairuhusiwi kunyoa mitindo.
9. Hairuhusiwi kunyoa vipara.
10. Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na vya jeshi.
11. Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda isiyoendana na vazi rasmi la shule.
12. Mashati makubwa sana na slim fit hayaruhusiwi.

9.0 MALI YA SHULE

1. Mwanafunzi akikabidhiwa vifaa kama vitabu vya kusomea anatakiwa kuviangalia sana na sharti avirudishe kwa mwalimu aliyemkabidhi kila vinapohitajika kurudishwa
2. Ieleweke kwamba ni kosa kubwa sana kuharibu mali yoyote ya shule ikiwa pamoja na majengo. Adhabu yake ni kufukuzwa shule.
3. Kifaaa chochote kitakachopotea sharti kilipwe. Cheti cha kumaliza shule hakitatolewa kwa yeyote ambaye hatarudisha au kulipa vifaa vyake.
4. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na begi lake la kuhifadhia vitabu vyake hairuhusiwi kubeba madaftari mkononi, mwanafunzi ana dhamana ya kutunza begi lake mwenyewe.

10.0 MIPAKA YA SHULE

Ni wajibu kila mwanafunzi kujua eneo lote la shule na mipaka yake. Maeneo yafuatayo yanahesabika kuwa ni nje ya mipaka ya shule

a. Chumba cha walimu (staff room) na vyumba vingine vya idara mbalimbali.
b. Maabara ya sayansi.
c. Ofisi wa utawala na ghala zote.
d. Jikoni.
e. Maeneo ya miradi.
f. Nyumba za walimu.
g. Nje ya Dar es salaam.
h. Eneo ambalo halijaendelezwa.

Kwa kuwa shule hii ni ya kutwa wanafunzi wanakaa sehemu mbalimbali za jiji la Dar es salaam nje ya mipaka ya shule. Kwa hiyo ipo haja ya kuwa na uhakika wa mahudhurio mazuri ya wanafunzi shuleni ili kudhibiti ufanisi wa program ya shule. Hivyo basi mwanafunzi anapaswa kubaki Dar es salaam hata siku ambazo si za masomo, isipokuwa wakati wa likizo kwa siku ambazo hana zamu shuleni.

RUHUSA YA KUTOKA NJE YA SHULE AU NJE YA DAR ES SALAAM.

a. Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda Fulani au wa siku inatolewa na mwalimu wa zamu kwa pasi
b. Ruhusa za kutoka nje ya Dar es salaam itatolewa na makamu mkuu wa shule kwa pasi
c. Apatapo ruhusa ya shule, Mwanafunzi anapaswa kurudi mapema
d. Ruhusa ya kwenda hospitali inaanzia kwa kupewa ruhusa kwa mwalimu wa darasa.

11.0 MAELEZO YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a. Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
b. Fomu ya binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule
d. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

MWISHO

Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema ya kujiunga na shule yetu. Ni matumaini yetu utazingatia kanuni na sheria za shule ili lengo lililokuleta shuleni liweze kukamilika, kauli yetu kwa pamoja

ELIMU KWA MAFANIKIO

_____

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI TOANGOMA,

S.L.P 100221

DAR ES SALAAM

MOB:- 0754 864590

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SEKONDARI YA TOANGOMA

S.L.P 100221, DAR ES SALAAM.

FOMU YA KUANDIKISHA SHULENI

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI

Jina kamili la mwanafunzi ……
Tarehe ya kuzaliwa ……
Wilaya aliyozaliwa …….
Uraia …… Dini ……
Mahali anakoishi mwanafunzi ……
Shule aliyokua anasoma kabla ya kuja Toangoma Sekondari

Picha ya mwanafunzi

Shule ya Sekondari/ msingi	Tarehe na mwaka ulioanza	Tarehe na mwaka uliotoka
i) ……..	……	……

Saini ya mwanafunzi _____ Tarehe_____

B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI

Jina kamili la mzazi/ mlezi ……..
Uraia …….
Anuani ya Dar es salaam …….
Sehemu anayoishi ……
Mtaa ……..
Namba ya nyumba ……
Simu: Nyumbani ……... Ofisini ……...
Eleza kama mototo ana matatizo yoyote ya kiafya ……...
……

Picha ya mzazi/mlezi

C. MAELEZO YA KIKAZI

i) Jina la mwajiri ……...
ii) Anuani ……...
iii) Kazi ya mzazi/ mlezi …….
(mfano: karani, mwalimu N.k)
Saini ya mzazi au mlezi …….. Tarehe ……

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Toangoma,
S.L.P 100221
Dar es salaam

Mimi …… (jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha …… mwaka …… katika shule ya Sekondari Toangoma.

Ninaahidi kwamba

1. Nitatii sharia za shule nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli za kishule.
3. Nitashiriki kikamilifu katikashughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyo bora bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza maligali (raw material) ya kuzalisha mali.
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu mkakamavu na madhumuni kuipa na kuitunza sifa ya shule ya Sekondari Toangoma.

"MUNGU NISAIDIE"

Saini ya Mwanafunzi ……..

Mimi (jina la mzazi/ mlezi) ……

Naahidi kwamba:-

1. Nitampa mwanangu mahitaji ya shule kama ilivyotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msada wowote utakao hitajika wa (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamuhimiza mwanangu kufanya mazoezi ya masomo ya nyumbani (home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Naaidhinisha mwanangu awapo shuleni ahudhurie vipindi vya dini ya …… Dhehebu la ……. Saini ……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TOANGOMA SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by the Government Medical Officer and returned to the HEAD OF SCHOOL TOANGOMA SECONDARY SCHOOL, P.O BOX 100221, DAR ES SALAAM.

To the Medical officer

……..

……..

A: RE ……

Please examine the above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below:

Say YES or No to each problem

……
HEADMASTER

i)	Hearing	Yes____	No____
ii)	Speech	Yes____	No____
iii)	Sight	Yes____	No____
iv)	T.B	Yes____	No____
v)	T.P	Yes____	No____
vi)	Diabetes	Yes____	No____
vii)	Mental Case	Yes____	No____
viii)	Physical Disability	Yes____	No____
ix)	Any other	Yes____	No____
x)	……		

B. Recommended if the student is fit for studentship (i) YES (ii) NO

……

C. Any other advise ……

Name and signature ……..

Date ……